AfyaMtandao Newsletter
No 02 - Oktoba 2008

Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC)

AfyaMtandao Newsletter
No 02 - Oktoba 2008

Karibu Afyamtandao!!

Bw. Petro Masatu Pamba,
Mratibu Afyamtandao

Kila kitu huanza kama wazo, hujengwa kwa kufikiri zaidi, pia hisia hatimaye utashi huhitajika kwa utekelezaji.

Tuna kila sababu za kuwashukuru wale wote ambao wameunga mkono juhudi hizi,kwa sasa tuko mahali safari tumeianza. Ombi langu tusimuangalie Rubani au Dreva peke yake,tukumbuke nasi kama abiria tunamchango mkubwa wa kuifanikisha safari hii.Mungu wetu ni yuleyule kwa Dunia nzima naamini atazibariki juhudi hizi.

KWA PAMOJA TUTAJENGA TAIFA JIPYA LENYE HUDUMA BORA ZA AFYA.

TEKNOHAMA inawezekana kinachohitajika ni kuchukua uamuzi na hatua!!

Mungu wetu aliyejaa neema awabariki kwa utayari wenu.

Hospitali ya Butimba na matumizi ya Kompyuta

Matumizi ya Kompyuta katika Dunia ya sasa ya utandawazi, imekuwa ni suala muhimu kwa Maendeleo ya jamii na yamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma ya afya kwenye hospitali,Vituo vya Afya na Zahanati.

Hospitali ya Butimba iliyopo katika Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza, ni moja kati ya hospitali ambazo zimeingia katika mfumo wa kutoa huduma ya afya kwa njia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) na kufanya huduma katika hospitali hiyo kuwa bora na yenye tija kwa Maendeleo ya Taifa.



Dkt.Beatrice Lubengula Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo anasema, tangu hospitali hiyo ilipoanza kutumia mfumo huo kuna mabadiliko makubwa ambayo yamepatikana ikiwemo pamoja na kuongezeka kwa mapato, kupunguza msongamano kwa kusajili wagonjwa kwa kutumia njia ya mtandao badala ya kuandika katika daftari kama ilivyokuwa awali.

Aidha, Bi.Auleria Marco Afisa Muuguzi wa hospitali hiyo anasema, mfumo huu umerahisisha sana katika utayarishaji wa ripoti ya Mwezi kwani hapo kabla utayarishaji wa ripoti ulichukua wiki moja au mbili kukamilika lakini sasa kupia mfumo huu ripoti inaandaliwa kwa muda mfupi na inakamilika kwa umakini mkubwa.

Pamoja na urahisi huo,Bi Auleria anasema kuna changamoto ambazo wanakutana nazo ikiwa ni pamoja na tatizo la umeme kukatika, upungufu wa watumishi na Muda wa kuhudhuria mafunzo ya Software hiyo.

Anasema kama Changamoto hizo zitafanyiwa kazi, basi utoaji huduma katika hospitali hiyo utaendelea kuimarika kwa kiwango kikubwa zaidi.Butimba ni hospitali iliyo katika maandalizi ya kuwa hospitali ya Wilaya na inamilikiwa na serikali.

PICHA: Washiriki wa HMIS wakiangalia mfumo wa AfyaPro

AfyaMtandao
Newsletter
No 02 - Oktoba 2008

KCMC yatoa mawe kwa darubini!

HOSPITALI ya Rufaa ya KCMC iliyopo mjini Moshi mkoani Kilimanjaro kwa kushirikiana na Hospitali ya North Umbria Health Trust wameanza kutoa huduma ya kutoa mawe kwenye mfuko wa nyongo kwa kutumia upasuaji wa kutumia darubini.

Mkuu wa Kitengo cha Upasuaji hospitalini hapo, Dk Chilonga Kondo, ameyasema hayo baada ya kuwafanyia upasuaji wagonjwa 14 wenye ugongwa huo hospitalini hapo.

Amesema upasuaji huo ni tofauti na uliokuwa ukitumiwa kipindi cha nyuma ambapo mgonjwa alikuwa akipasuliwa sehemu kubwa ya tumbo, hivyo kupata maumivu makali na kuchukua muda mrefu kupona.

Dk. Kondo amesema upasuaji kwa kutumia teknolojia hiyo mpya, mgonjwa anachukua saa 24 hadi 48 hivyo anapata nafuu mapema na kuweza kula, pamoja na kufanya mazoezi ya kutembea.

Amesema upasuaji huo unawasaidia wagonjwa kupona haraka na hivyo kuruhusiwa mapema na hali hiyo inawasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini hapo.

Dk. Kondo amesema tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo Novemba mwaka 2004, wagonjwa 36 wameshafanyiwa upasuaji huo na kuongeza kuwa njia hiyo pia itasaidia kuondoa ugonjwa wa kidole tumbo.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za hospitali hiyo, Dk. Mark Swai, amesema madaktari wengi katika hospitali hiyo hawana utaalam huo na kwamba hospitali inatumia chombo maalum wakati wa upasuaji ambacho kina uwezo wa kutoa maelezo na kuwasiliana na wataalam wa Uingereza, ili kutoa msaada wa maelekezo ya upasuaji huo.

Itwana's profile



Ernest Itwana ni Msimamizi wa mifumo ya Kompyuta (Sytems Administrator) Kitengo cha Afyamtandao na Tume ya Kikristo ya huduma za jamii (CSSC).Ni Mtaalamu wa Kompyuta na Mtandao (Internet).Baada ya kumaliza Diploma ya Kompyuta katika Chuo cha Desktop Computer Technology (DCT) cha Jijini Dar es salaam na kufanya mazoezi kwa njia ya vitendo (Field Attachment) katika Bodi ya Taifa ya ugavi (NBMM) na University Computing Centre (UCC) Amejiunga na CSSC-Afyamtandao akiwa na ujuzi wa kutosha katika TEKNOHAMA (ICTs).Kwa msaada zaidi wasiliana naye kwa Barua pepe; eitwana@afyamtandao.org au eitwana@cssc.or.tz

AfyaMtandao
Newsletter
No 02 - Oktoba 2008

Kuboresha TEKNOHAMA kwenye Kanda

Tume ya Kikristu ya huduma za jamii (CSSC) kupitia kitengo cha TEKNOHAMA (ICT),imedhamiria kuboresha teknolojia ya TEKNOHAMA kwenye kanda zote ambazo inahudumia.Hali hii imetokana na kuendesha zoezi la kufanya tathimini ya mahitaji yanayohitajika katika katika kuboresha teknolojia hii.

Kanda ambazo zeozi hili limefanyika ni pamoja na kanda ya kusini,kanda ya ziwa,kanda ya Mashariki,Kaskazini na Magharibi.

Mkuu wa kitengo cha TEKNOHAMA,CSSC ambaye pia ni Mratibu wa Afyamtandao Bw.Petro Masatu Pamba amesema zoezi hili limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani mambo muhimu katika kuboresha teknolojia hii kwenye kanda yaliainishwa na wahusika wakuu kutoka katika Kanda hizo,mambo hayo ni pamoja na kuhitajika kwa mafunzo ya kutosha kwa watumishi katika zone hizo,kuwepo na Software Uboreshwaji wa TEKNOHAMA unahitajika kwa kiwango kikubwa kwenye ofisi za Kanda ili kusaidia katika kuandaa, kukusanya na

kutoa taarifa mbalimbali,kwani TEKNOHAMA inatumika katika kusimamia ugawaji wa madawa,mishahara,kurekodi taarifa za afya,upimaji,matibabu na kusaidia katika Mafunzo.

Wanachama wa Afyamtandao

Wanachama wa Afyamtandao wamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni;

Wanachama washiriki (Corporate members)

Kundi hili la Wanachama linajumuisha watu kutoka idara za serikali kuu na zile za Mitaa,Mashirika yasiyo ya kiserikali,Mashirika ya Dini,Mashirika ya Wataalam yakijumuisha sekta binafsi za Afya.Watumiaji wote wa huduma ya TEKNOHAMA ni wanachama washiriki.

Wanachama wataalamu

Hawa ni wafanyakazi wa Afya wanaojumuisha Wataalamu wa Afya kutoka moja kwa moja kwenye sekta ya Afya na Wataalamu wa TEKNOHAMA.

Wanachama waanzilishi

Kundi hili linaundwa na waanzilishi wa Afyamtandao ambao ni Tume ya Kikristo ya huduma za jamii (CSSC).

AfyaMtandao
Newsletter
No 02 - Oktoba 2008

Watoa huduma za Afya Majumbani na washauri nasaha wapewa Mafunzo

Tume ya Kikristo ya huduma za jamii (CSSC) kupitia mradi wake wa HIV/AIDS Global Fund kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa kudhibiti Ukimwi (NACP),imeendesha

mafunzo ya watoa huduma za afya Majumbani na ushauri nasaha kwa watoa huduma wa afya wanaotoa huduma zao katika vituo vya afya vinavyoendeshwa na makanisa.

Malengo makuu ya mafunzo hayo yalikuwa ni kupanua na kuboresha maarifa,ujuzi na muelekeo chanya kwa watoa huduma hao na washauri nasaha kuhusiana na suala zima la kuwahudumia na kuwasaidia watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi ikiwa ni pamoja na huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya Ukimwi (VCT).

Vilevile mafunzo yalilenga zaidi kuwawezesha wahusika kuwa na ujuzi wa ambao utasaidia kutoa ushauri nasaha kwa watu wanaishi na virusi vya Ukimwi na kutumia mafunzo hayo pia katika kumuhudumia Mgonjwa nyumbani.

Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa njia ya kushirikishana baina ya wakufunzi na wanafunzi ambapo kila mshiriki alipata nafasi ya kuchangia mada iliyojadiliwa kwa kutoa uzoefu wake ambao amekutana nao katika shughuli zake.

Mwisho wa mafunzo hayo washiriki walipendekeza CSSC na wadau wengine kutembelea na kufanya tathimini kuona matokeo ya mafunzo hayo kwa wahusika jinsi yalivyowasaidia na kuendelea kutoa mafunzo zaidi kwa wahudumu wa afya ili kuboresha huduma za afya nchini.

Tiba Mtandao kwa Maendeleo ya Taifa

CSSC-Afyamtandao kupitia kitengo cha Media kwa kushirikiana na mradi wa mawasiliano wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT) dayosisi ya kaskazini imetengeneza filamu ndogo inayoonyesha jinsi huduma ya Tibamtandao inavyofanyika kwa baadhi ya hospitali za kanda ya Kaskazini na Kusini katika Mikoa ya Kiliman jaro,Arusha,Manyara na Iringa.

Filamu hiyo ya Dakika kumi iliyodhaminiwa na Taasisi ya Kimataifa ya Mawasiliana na Maendeleo (IICD),inaonyesha jinsi Tiba Mtandao inavyosaidia wagonjwa kupata huduma ya rufaa sehemu yeyote walipo na kuokoa gharama za kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma hiyo.

Baadhi ya hospitali ambazo filamu hii imetengenezwa ni pamoja na hospitali ya Rufaa ya KCMC,hospitali za Ngoyoni,Marangu na Seliani zinazomilikiwa na Kanisa la KKKT na St.Elizabethi inayomilikiwa na Kanisa Katoliki.

Huduma hii kwa ukanda huo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa ambapo matatizo mbalimbali ya wagonjwa yamekuwa yakishughulikiwa kwa Muda mfupi na kwa haraka zaidi.Mgonjwa anapofika hospitali na kuonekana kuwa tatizo lake ni kubwa daktari muhusika anachukua vipimo vya mgonjwa huyo na kuvituma kwa madaktari wengine, yaweza kuwa ni hospitali ya rufaa kwa ushauri zaidi wa kitaalamu,na majibu yanapatikana na Mgonjwa anapata tiba inayostahili kwa muda unaotakiwa.

Filamu hii itasambazwa kwa wadau mbalimbali wa Afya kwa lengo la kushirikishana utaalamu na Maarifa.

Wasiliana na Afyamtandao:
S.L.P 9433
DAR ES SALAAM
TANZANIA
SIMU: +255 22 2112918; 2123730
MOBILE: 0755393624, 0754770866, 0784412091
BARUA PEPE: afyamtandao@afyamtandao.org
TOVUTI: www.afyamtandao.org

iicd
People - ICT - Development

AfyaMtandao
Newsletter
No 02 - Oktoba 2008

TCMA yahudumia Afya kwa asilimia 40

CHAMA cha madaktari Wakristu Tanzania (TCMA)kimesema kimefikia kutoa huduma za afya kwa jamii kgwa asilimia 40 wakati Serikali na vituo vya afya vya watu binafsi vinatoa huduma hiyo kwa asilimia 60.

Mwenyekiti wa chama hicho Dkt. Isaya Tosiri alisema hayo mjini Dar es salaam wakati wa ufunguzi wa mkutano wa 71 wa madaktari wa wakristo waliokuwa wanajadili huduma ya afya inayopatikana nchini.

Dkt.Tosiri alisema madaktari wakristo wanatoa ushirikiano mkubwa na kuomba vituo vingine vya afya vya watu binafsi na serikali kusaidiana kwa pamoja ili kupunguza matatizo ya wagonjwa.

" Kwa kweli endapo tukiwa tunashirikiana katika suala la huduma ya afya matatizo ambayo yanawakabili wagonjwa yatapungua na tuachane na hali ya kujali maslahi zaidi bali tufanye kazi" alisema Dkt. Tosiri.

Alisema kuwa chama hicho kimefanya utafiti na kugundua kwamba watoto 700 wanaozaliwa nchini wana ulemavu wa mdomo (Cleft lip and palate).

Alisema jumla ya watoto 200,000 katika nchi zinazo endelea na zilizo chini ya jangwa la sahara wanazaliwa kila mwaka wakiwa na tatizo la ulemavu wa mdomo na kusisitiza kuwa ugonjwa huo ni hatari kwa mtoto.

Ulemavu huo unatibika kwa njia ya upasuaji,lakini wazazi wengi wanashindwa kumudu gharama.

Mradi ya AfyaMtandao ambao uko chini ya Tume ya Kikristu ya huduma za jamii (CSSC) ulitambulishwa kwa wajumbe.

Dkt.Isaya Tosiri akihutubia katika mkutano wa 71 wa TCMA TEC Dar es Salaam

Zahanati ya Nassa yaboresha huduma

Huduma ya Afya kwa baadhi ya hospitali,Vituo vya Afya na Zahanati za Kanda ya ziwa imezidi kuimarika zaidi baada ya mfumo wa kuhifadhi taarifa kwa njia ya kompyuta kupitia programu ya Afya- pro kuanza kutumika katika vituo hivyo.

Zahanati ya Nassa ambayo inamilikiwa na Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT),baada ya kuanza kutumia mfumo huo,imefanikiwa kuboresha huduma zake kwa kiwango kikubwa.

Rachel Paul Muuguzi katika Zahanati hiyo ambaye pia hukaimu nafasi ya Mganga Mkuu kituoni hapo anasema, tangu mfumo huu uanze kufanyakazi katika zahanati hiyo umesaidia katika kuhifadhi takwimu na taarifa kwa ubora zaidi bila upotevu ikilinganishwa na kipindi cha nyuma ambapo kazi nyingi zilifanyika kwa njia ya kuandika kwa mkono,hali ambayo ilipelekea ugumu wa kazi hasa wakati wa kuandaa ripoti.

Rachel anasema kwa sasa mfumo huo unasaidia katika kuandaa ripoti zilizo safi ambazo hupelekwa wilayani na wao huzitumia katika kupanga na kuandaa bajeti zao za mwaka katika kununua madawa na shughuli zingine za maendeleo kituoni hapo.

Anasema, mfumo huo umechangia kupunguza idadi ya wagonjwa kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu wakisubiri kupata huduma hii inatokana na mfumo kuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi kwa muda mfupi, kumekuwa pia na ongezeko kubwa la mapato ambapo mfumo una sehemu maalumu ya kuhesabu malipo yote yanayolipwa kituoni hapo hivyo unaondoa udanganyifu.

Amezitaja sehemu ambazo zimeunganishwa na mfumo huo wa Kompyuta kuwa ni pamoja na Mapokezi, Ofisi ya Mganga Mkuu, Maabara, Idara ya Malipo (Billing) na Bohari ya madawa.Ameongeza kuwa kila idara inafanyakazi kwa ufanisi mkubwa kwa kutumia mfumo huo.

Zahanati ya Nassa iko wilaya ya Magu katika Mkoa Mwanza Kanda ya Ziwa.

Sikiliza!!
96.1 Radio SAUT fm
Mwanza - Tanzania